**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA**
*(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)*

Mkoa wa Shinyanga
Simu: 028 – 2710182
Fax Na: 028 - 2710504
ded.msalaladc@shinyanga.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S. L. P. 16,
**KAHAMA.**

Unapojibu Tafadhali taja:

*Tarehe 29/04/2021*

*Kumb Na.* MDC/E.60/02/109

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Msalala kupitia kibali cha ajira mbadala chenye Kumb.Na.FA.170/376/01/"B"/46 cha tarehe 06 April, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa kujaza nafasi zifuatazo:-

**2. MTENDAJI WA KIJIJI III – NAFASI MOJA (1)**

**2.1. Sifa za Muombaji,**

Awe na elimuya kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali

**2.2. Ngazi ya Mshahara**

TGS. B, kwa kuzingatia viwango vya Serikali

**2.3. Majukumu ya Kazi**

I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
II. Kusimamia Ulinzi na Utawala Bora kwa Raia na mali zao. Kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
III. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika Kijiji
IV. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji

IV. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji

V. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu

VI. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.

VII. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji

VIII. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbuu zote na nyaraka za Kijiji

IX. Kuwa mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika Kijiji

X. Kupokea,kusikiliza na kutatua migogoro ya wananchi

XI. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na

XII. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

**3. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II – NAFASI MOJA (1)**

**3.1. Sifa za Muombaji,**

I. Awe amehitimu kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) na mwenye cheti cha utunzaji kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

**3.2. Ngazi ya Mshahara,**

TGS.B Kwa kuzingatia viwango vya serikali

**3.3. Majukumu ya Kazi,**

I. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanayohitajika na wasomaji

II. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka

III. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification of boxing) kwaajili ya matumizi ya Ofisi

IV. Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki ( file racks/cabinets) katika masjala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu

V. Kuweka kumbukumbu (barua,nyaraka n.k.) katika mafaili

VI. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu /nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.

**4. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE**

I. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wanye umri usiozidi miaka 45

II. Waombaji waambatanishe cheti cha kuzaliwa

III. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wa kuaminika

IV. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma,maelezo na vyeti vya kidato cha Nne na Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

V. ***Testimonials, "Provision Results", "Statements of Results", hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita HAVITAKUBALIWA***

VI. Waombaji waambatishe picha moja "Pasport Size" ya hivi karibuni

VII. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **13/05/2021**

NB; Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ded@msalaladc.go.tz tovuti ya secretarieti ya ajira www.ajira.go.tz na katika mbao za matangazo za Halmashauri

**Maombi yote yatumwe kwa:**

*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya Msalala*
*S.L.P 16*
*KAHAMA*

S.S.Berege
MKURUGENZI MTENDAJI
**MSALALA-KAHAMA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MSALALA